**Vituo vya Afya vya Jamii vya Burlington, Inc.**

*617 Riverside Avenue*
*Burlington, VT 05401*
*802) 864-6309*
*www.chcb.org*



# Maelezo yako. Haki Zako. Majukumu Yetu.

Ilani hii inaelezea jinsi maelezo ya matibabu kukuhusu yanaweza kutumiwa na kufichuliwa na jinsi unaweza kufikia maelezo haya. **Tafadhali ipitie kwa makini.**

## Haki Zako

**Inapohusu maelezo yako ya afya, una haki maalum.** Sehemu hii inaelezea haki zako na baadhi ya majukumu yetu ya kukusaidia.

| | |
|---|---|
| **Kupata nakala ya kielektroniki au ya karatasi ya rekodi yako ya matibabu** | • Unaweza kuomba kuona au kupata nakala ya kielektroniki au ya karatasi ya rekodi yako ya matibabu na maelezo mengine ya afya tunayo kukuhusu. Tuulize jinsi ya kufanya hivi.<br>• Tutatoa nakala au muhtasari wa maelezo yako ya afya, kwa kawaida, ndani ya siku 30 baada ya maombi yako. Tunaweza kulipisha ada inayoeleweka inayohusiana na gharama. |
| **Kutuomba tusahihishe rekodi zako za matibabu** | • Unaweza kutuomba tusahihishe rekodi ya afya kukuhusu ambayo unadhania si sahihi au si kamili. Tuulize jinsi ya kufanya hivi.<br>• Tunaweza kusema “hapana” kwa maombi yako, lakini tutakuelezea kwa nini kwa kukuandikia ndani ya siku 60. |
| **Kuomba mawasiliano ya siri** | • Unaweza kutuomba tuwasiliane na wewe kwa njia fulani (kwa mfano, simu ya nyumbani au ya ofisini) au tutume batua kwa anwani tofauti.<br>• Tutakubali maombi yote yanayoeleweka. |

*inaendelea kwenye ukurasa unaofuata*

## Haki Zako, *kuendelea*

| | |
|---|---|
| **Kutuomba tupunguze tunachotumia au kushiriki** | • Unaweza kutuomba tusitumie au kushiriki maelezo mengine ya afya kwa matibabu, malipo au shughuli zetu.<br>    • Hatuhitajiki kukubaliana na maombi yako, na tunaweza kusema “hapana” kama inaweza kuathiri huduma yako.<br>• Ukilipia kikamilifu huduma au bidhaa ya huduma ya afya kutoka kwa mfuko wako, unaweza kutuomba tusishiriki maelezo hayo kwa malengo ya malipo au shughuli zetu na mtoa huduma wako wa afya.<br>• Tutasema “hapana” isipokuwa sheria inahitaji ushiriki maelezo hayo. |
| **Kupata orodha ya wale ambao tumeshiriki maelezo** | • Unaweza kuomba orodha (hesabu) ya mara ambazo tumeshiriki maelezo yako ya afya kwa miaka sita kabla ya tarehe unayoomba, tulishiriki na nani, na kwa nini.<br>• Tutajumuisha fichuzi zote isipokuwa zile zinazohusu matibabu, malipo, na shughuli za huduma ya afya, na fichuzi nyingine (kama yoyote uliyotuomba tufanye). Tutatoma hesabu moja kwa mwaka bila malipo lakini tutatoza ada inayofaa inayotegemea gharama ikiwa utaomba nyingine ndani ya miezi 12. |
| **Kupata nakala ya ilani hii ya faragha** | • Unaweza kuomba nakala ya karatasi ya ilani hii wakati wowote ule, hata kama umekubali kupokea ilani kwa njia pepe. Tutakupa nakala ya karatasi mara moja. |
| **Kuchagua mtu wa kutenda kwa niaba yako** | • Ikiwa umempa mtu nguvu za matibabu za wakili au ikiwa mtu ni mlezi wako wa kisheria, mtu huyo anaweza kutumia haki zako na kufanya maamuzi kuhusu maelezo yako ya afya.<br>• Tutahakikisha mtu huyo ana mamlaka haya na anaweza kutenda kwa niaba yako kabla tuchukue hatua yoyote. |
| **Kuwasilisha malalamiko ukihisi haki zako zinakiukwa** | • Unaweza kulalamika ikiwa unahisi tumekiuka haki zako kwa kuwasiliana nasi kwa kutumia maelezo kwenye ukurasa wa 1<br>• Unaweza kuwasilisha malalamiko kwa Ofisi ya Idara ya Marekani ya Afya na Huduma za Binadamu ya Haki za Raia kwa kutuma barua kwa 200 Independence Avenue, S.W., Washington, D.C. 20201, kupiga simu 1-877-696-6775, au kutembelea **www.hhs.gov/ocr/privacy/hipaa/complaints/.**<br>• Hatutalipiza kisasi kwa kuwasilisha malalamiko. |

## Chaguo Zako

**Kwa maelezo mengine ya afya, unaweza kutuambia chaguo zako kuhusu tunachoshiriki.** Ikiwa una upendeleo wazi wa jinsi tunavyoshiriki maelezo yako katika hali zilizoelezwa hapa chini, ongea nasi. Tueleze unachotaka tufanye, na tutafuata maagizo yako.

| | |
|---|---|
| **Katika hali hizi, una haki na chaguo la kutuambia:** | • Tushiriki maelezo na familia yako, marafiki wa karibu, au wengine wanaohusika katika huduma yako<br>• Tushiriki maelezo katika hali ya kutoa misaada.<br>• Tujumuishe maelezo yako katika saraka ya hospitali.<br>• Tuwasiliane na wewe kwa juhudi za kuchangisha fedha<br>*Ikiwa huwezi kutuambia mapendeleo yako, kwa mfano ikiwa umepoteza fahamu, tunaweza kuendelea na tushiriki maelezo yako ikiwa tunaamini ni kwa manufaa yako. Tunaweza pia kushiriki maelezo yako wakati yanahitajika ili kupunguza makali na tishio kwa afya au usalama.* |
| **Katika hali hizi hatushiriki *kamwe* maelezo yako isipokuwa utupatie kibali kilichoandikwa:** | • Malengo ya matangazo<br>• Mauzo ya maelezo yako<br>• Kushiriki vidokezo vya matibabu ya kisaikolojia |
| **Katika hali ya kuchangisha fedha:** | • Tunaweza kuwasiliana na wewe kwa juhudi za kuchangisha fedha, lakini unaweza pia kutuambia tusiwasiliane na wewe tena. |

## Matumizi na Ufichuzi Wetu

**Kwa kawaida tunatumia na kushiriki aje maelezo yako ya afya?** Kwa kawaida tunatumia au kushiriki maelezo yako ya afya kwa njia zifuatazo.

| | | |
|---|---|---|
| **Kukutibu** | • Tunaweza kutumia maelezo yako ya afya na kuyashiriki na wataalamu wengine wanaokutibu. | ***Mfano:*** *Daktari anayekutibu jeraha akiuliza daktari mwingine kuhusu hali ya afya yako kwa ujumla.* |
| **Kuendesha shirika letu** | • Tunaweza kutumia na kushiriki maelezo yako ya afya ili kuendesha shughuli yetu, kuboresha huduma yetu, na kuwasiliana na wewe ikihitajika. | ***Mfano:*** *Tunatumia maelezo ya afya kukuhusu ili kudhibiti matibabu na huduma zetu.* |
| **Bili ya huduma zako** | • Tunaweza kutumia na kushiriki maelezo yako ya afya ili kutengeneza bili na kupata malipo kutoka kwa mipango ya afya au mashirika mengine. | ***Mfano:*** *Tunatoa maelezo kukuhusu kwa mpango wako wa huduma ya afya ili iweze kulipia huduma zako.* |

*kuendelea kwenye ukurasa unaofuata*

## Ni kwa njia gani nyingine tunaweza kutumia au kushiriki maelezo yako ya afya?

Tunaruhusiwa au tunahitajika kushiriki maelezo yako kwa njia zingine - kwa kawaida kwa njia ambazo zinachangia manufaa ya umma, kama vile afya na utafiti wa umma. Lazima tutimize masharti mengi katika sheria kabla tuweze kushiriki maelezo yako kwa malengo haya.
Kwa maelezo zaidi angalia: **www.hhs.gov/ocr/privacy/hipaa/understanding/consumers/index.html.**

| | |
|---|---|
| **Msaada wa afya ya umma na masuala ya usalama** | • Tunaweza kushiriki maelezo ya afya kukuhusu kwa hali zingine kama vile:<br>• Kuzuia maradhi<br>• Kusaidia katika kurejesha bidhaa<br>• Kuripoti madhara mabaya ya dawa<br>• Kuripoti matumizi mabaya yanayoshukiwa, upuuzaji, au mzozo wa kinyumbani<br>• Kuzuia au kupunguza tishio kubwa kwa afya au usalama wa mtu yeyote |
| **Kufanya utafiti** | • Tunaweza kutumia au kushiriki maelezo yako kwa utafiti wa afya. |
| **Kutii sheria** | • Tutashiriki maelezo kukuhusu ikiwa sheria za jimbo au serikali zinaihitaji, ikiwa ni pamoja na Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ikiwa inataka kuona kwamba tunatii sheria ya siri ya serikali. |
| **Kujibu maombi ya kutoa viungo na tishu** | • Tunaweza kushiriki maelezo ya afya kukuhusu na mashirika ya yanayoshughulikia utoaji viungo. |
| **Kufanya kazi na mchunguzi wa matibabu au mkurugenzi wa chumba cha kuhifadhia maiti** | • Tunaweza kushiriki maelezo ya afya na mpelelezi, mchunguzi wa matibabu, au mkurugenzi wa chumba cha kuhifadhia maiti wakati mtu anapokufa. |
| **Kushughulikia fidia ya wafanyakazi, kutekeleza sheria, na maombi mengine ya serikali** | • Tunaweza kutumia au kushiriki maelezo afya kukuhusu:<br>• Kwa madai ya fidia ya wafanyakazi<br>• Kwa malengo ya kutekeleza sheria au na afisa wa kutekeza sheria<br>• Na mashirika ya kusimamia afya kwa shughuli zilizoidhinishwa na sheria<br>• Kwa kazi maalum za serikali kama vile jeshi, usalama wa taifa, na huduma za kumlinda rais. |
| **Kujibu mashtaka na hatua za kisheria** | • Tunaweza kushiriki maelezo ya afya kukuhusu kwa kujibu amri ya mahakama au ya utawala, au kwa kuitikia shurutisho. |

*Rekodi za Matibabu ya Matumizi Mabaya ya Dawa za Kulevya na Pombe: Vituo vya Afya vya Jamii vya Burlington, Inc. ("CHCB") havitatoa rekodi zozote za matibabu ya matumizi mabaya ya dawa za kulevya au pombe chini ya sheria ya 42 CFR Sehemu ya 2 ("Sehemu ya 2") bila idhini iliyoandikwa kutoka kwa mgonjwa au mwakilishi wake wa kisheria ambayo inatimiza mahitaji ya ufichuzi. Ikiwezekana, CHCB itachukua hatua ya kuondoa shurutisho kwa maelezo yaliyoshughulikiwa chini ya Sehemu ya 2 kama inavyohitajika na sheria.*

*Vidokezo vya matibabu ya kisaikolojia: Kulingana na Sheria ya Jimbo la Vermont, Vituo vya Afya vya Jamii vya Burlington, Inc havitafichua vidokezo vyovyote vya matibabu ya kisaikolojia isipokuwa mgonjwa aombe hasa kwa kuandika kama sehemu ya idhini halali ya kufichua maelezo kwamba vidokezo hivyo vinapaswa kutolewa.*
*Hii inamaanisha kwamba idhini inayoomba "rekodi nzima ya matibabu" HAITAJUMUISHA vidokezo vya matibabu ya kisaikolojia isipokuwa iwe imeombwa kimahususi.*

## Majukumu Yetu

- Tunahitajika kisheria kudumisha faragha na usalama wa maelezo yako yaliyolindwa ya afya.
- Tutakufahamisha mara moja ikiwa ukiukaji utatokea ambao unaweza kuhatarisha faragha au usalama wa maelezo yako.
- Lazima tufuate kanuni za kazi na faragha zilizoelezewa katika ilani hii na tukupe nakala yake.
- Hatutamua au kushiriki maelezo yako isipokuwa kama ilivyoelezewa hapa isipokuwa utueleze kuwa tunaweza kwa kuandika. Ukituelezea tunaweza, unaweza kubadilisha nia yako wakati wowote. Tufahamishe kwa kuandika ukibadilisha nia yako.

Kwa maelezo zaidi angalia: **www.hhs.gov/ocr/privacy/hipaa/understanding/consumers/noticepp.html.**

### Mabadiliko kwa Masharti ya Ilani Hii

Tunaweza kubadilisha masharti ya ilani hii, na mabadiliko hayo yatatumika kwa maelezo yote tunayo kukuhusu. Ilani hiyo mpya itapatikana ukiomba, katika ofisi yetu, na kwenye tovuti yetu.

*Oktoba 24, 2013*

**Ilani Hii ya Kanuni za Faragha inatumika kwa mashirika yafuatayo.**

*maeneo yote ya Vituo vya Afya vya Jamii vya Burlington, Inc. pamoja na:*

- *Kituo cha Afya cha The Riverside*
- *Kituo cha Afya cha The Safe Harbor*
- *Kituo cha Afya cha Vijana cha The Pearl Street*
- *Kituo cha Afya cha The Keeler Bay*

*Afisa wa Faragha wa CHCB: Jonathan Bowley* | *Simu: (802) 264-8152* | *Barua pepe: jbowley@chcb.org*